Mahakama Tatu

na

Ellis Forsman

Mahakama Tatu

na

Ellis Forsman

Oktoba 15, 2011

Mahakama Tatu

1 Kor. 4:3-5

Miongoni mwa matatizo mengi ambayo yalikuwepo katika kanisa kule Korintho…

Kulikuwa na tatizo la mgawanyiko.

1 Kor. 1:10-11, "*Basi ndugu nawasii kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, nyote mnene mamoja wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja. Kwa maana ndugu zangu nimearifiwa habari zenu na wale walio wa nyumbani mwa Kloe, ya kwamba iko fitina kwenu.*"

Hii ilihusisha "utengano wa ubinafsi".

1 Kor. 1:12, "*Basi maana yangu ni hii ya kwamba kila mtu wa kwenu husema mimi ni wa Paulo, na mimi ni wa Apolo, na mimi ni wa Kefa, na mimi ni wa Kristo.*"

Katika kushughulikia tatizo, mtume Paulo…

Anakemea kutokukomaa kiroho wa mgawanyiko huo.

1 Kor. 3:1-4, "*Lakini ndugu zangu mimi sikuweza kusema nanyi kama na watu wenye tabia ya rohoni, bali kama na watu wenye tabia ya mwilini, kama na watoto wachanga katika Kristo. Naliwanywesha maziwa sikuwalisha chakula; kwa kuwa mlikuwa hamjakiweza. Naam, hata sasa hamkiwezi, kwa maana hata sasa ninyi ni watu wenye tabia ya mwilini. Maana ikiwa kwenu kuna husuda na fitina. Je! Si watu wa tabia ya mwilini ninyi; tena mnaenenda kwa jinsi ya kibinadamu? Maana mtu mmoja asemapo mimi ni wa Paulo; na mwingine mimi ni wa Apolo, je! Ninyi si wanadamu?*"

Imefunua jinsi mtu anavyoweza kutazama jukumu la wengine.

- 1 Kor. 3:5-9, "*Basi Apolo ni nani? Na Paulo ni nani? Ni wauhudumu ambao kwao mliamini; na kila mtu kama Bwana alivyompa. Mimi nilipanda Apolo akatia maji; bali mwenye kukuza ni Mungu. Hivyo, apandaye si kitu, wala atiaye maji, bali Mungu akuzaye. Basi yeye apandaye na yeye atiaye maji ni wamoja, lakini kila mtu atapata thawabu yake mwenyewe sawasawa na taabu yake mwenyewe.*

Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu; ninyi ni shamba la Mungu, ni jengo la Mungu."

- 1 Kor. 4: 1-2, "*Mtu na atuhesabu hivi, kuwa tu watumishi wa Kristo, na mawakili wa siri za Mungu. Hapo tena inayohitajika katika mawakili, ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu.*"

Anasifu kwamba katika swala lake mwenyewe alivutiwa sana na kile alichokifiria Bwana.

1 Kor. 4: 3-5, "*Lakini kwangu mimi si kitu kabisa nihukumiwe na ninyi, wala kwa hukumu ya kibinadamu, wala sijihukumu hata nafsi yangu. Maana sijui sababu ya kujishitaki nafsi yangu lakini sihesabiwi haki kwa sababu ya hiyo; ila anihukumuye mimi ni Bwana. Basi ninyi msihukumu neno kabla kabla ya wakati wake, hata ajapo Bwana ambaye atayamlikisha yaliyositirika ya giza, na kuyadhihirisha mashauri ya mioyo; ndipo kila mtu atakapoipata sifa yake kwa Mungu.*"

Katika kifungu cha somo hili (1 Kor. 4:3-5), tunatambulishwa katika aina tatu tofauti ya hukumu…

- Mahakama inayotolewa maamuzi na wanadamu.
- Mahakama inayotolewa maamuzi na dhamira ya mtu binafsi.
- Mahakama inayohukumiwa na Kristo.

Haya tunaweza kuyaita "Mahakama Tatu".

Katika mfumo wa mahakama zetu za kibinadamu, tuna…

- Mahakama ya mwanzo.
- Mahakama ya wilaya.
- Mahakama kuu ya taifa (ambayo jaji ndiye mtoa maamuzi ya mwisho).

Ndivyo ilivyo katika "Mahakama Tatu" ndani ya kifungu chetu. Kuna tofauti kati yao, na tunafanya vyema kuona kile ambacho maandiko yanasema kuhusu kila moja. Tunaanza na "mahakama" ya chini…

Mahakama inayotolewa maamuzi na wanadamu

Mtazamo wa Paulo juu ya "mahakama" hii…

1 Kor. 4:3, "*Lakini kwangu mimi <u>si kitu kabisa</u> nihukumiwe na ninyi, wala kwa hukumu ya kibinadamu…*"

Angalia kwa makini kwamba anasema "*si kitu kabisa*", si "chochote".

Mara nyingi Paulo aliangali kuhusu ambacho watu walifikiria kuhusu baadhi ya mambo.

Kuhusu ambacho ndugu yake mdhaifu alifikiria.

1 Kor. 8:13, "*Kwa hiyo chakula kikimkwaza ndugu yangu, hakika sitakula nyama hata milele, nisije nikamkwaza ndugu yangu.*"

Kuhusu ambacho waliopotea wanafiria.

- 1 Kor. 9:19-23, "*Maana ingawa nimekuwa huru kwa watu wote, nalijifanya mtumwa wa wote, ili nipate watu wengi zaidi. Nalikuwa kama Myahudi kwa Wayahudi ili niwapate Wayahudi; kwa wale walio chini ya sheria, nalikuwa chini ya sheria, (ingawa mimi mwenyewe si chini ya sheria), ili niwapate walio chini ya sheria. Kwa wale wasio na sheria nalikuwa kama sina sheria, (si kwamba sina sheria mbele za Mungu, bali mwenye sheria mbele za Kristo), ili niwapate hao wasio na sheria. Kwa wanyonge nalikuwa mnyonge, ili niwapate wanyonge. Nimekuwa hali zote kwa watu wate, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu. Nami nafanya mambo yote kwa ajili ya Injili ili kuishiriki pamoja na wengine.*"

- 1 Kor. 10:31-33, "*Basi mlapo au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu. Msiwakoseshe Wayahudi wala Wayunani wala kanisa la Mungu, vile vile kama mimi niwapendezavyo watu wote katika mambo yote, nisitake faida yangu mwenyewe, ila faida yao walio wengi, wapate kuokolewa.*"

Lakini kile ambacho watu walimfikiria kilikuwa "*si kitu kabisa*"…

Sababu ya mtazamo wa Paulo…

Alijua jinsi maoni ya wengine yanvyokuwa.

Ulimwengu unapenda waalimu wa uongo.

- Luka 6: 26, "*Ole wenu ninyi watu wote watakapowasifu, kwa kuwa baba zao waliwatenda manabii wa uongo mambo kama hayo.*"

- Yer. 5:30-31, "*Jambo la ajabu la kuchukiza, imetokea katika nchi hii! Manabii wanatabiri uongo, na makuhani wanatawala kwa msaada wa hao; na watu wangu wanapenda mambo yawe hivyo. Nanyi mtafanya nini mwisho wake?*"

Waliwachukia hao "siyo wa dunia".

Yoh. 15:18-19, "*Iwapo ulimwengu ukiwachukia, mwajua ya kuwa umenichukia mimi kabla ya kuwachukia ninyi. Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungewapenda walio wake; lakini kwa kuwa ninyi*

si wa ulimwengu, bali mimi naliwachagua katika ulimwengu, kwa sababu hiyo ulimwengu huwachukia."

Alifahamu kwamba tabia yao ya kuhukumu haikuwa sahihi.

Maranyingi waliangalia mtazamo wa nje.

1 Sam. 16:7, "*Lakini BWANA akamwambia Samweli, usimtazame uso wake, wala urefu wa kimo chake; kwa maana mimi nimemkataa. BWANA haangalii kama binadamu aangaliavyo; maana wanadamu huitazama sura ya nje, bali BWANA hutazama moyo.*"

Tatizo ambalo Paulo angekabiliana nalo.

- 2 Kor. 10:7, "*Yaangalieni yaliyo mbele ya macho yenu. Mtu akijitumaini mwenyewe ya kuwa ni mtu wa Kristo, na afikiri hivi pia nafsini mwake, ya kwamba kama yeye alivyo mtu wa Kristo, vivyo hivyo na sisi.*"
- 2 Kor. 10:10, "*Maana wasema, Nyaraka zake ni nzito, hodari; bali akiwapo mwenyewe mwilini ni dhaifu, na maneno yake si kitu.*"

Alfu pia alijua alichokisema Bwana.

Yoh. 7:24, "*Basi msihukumu hukumu ya macho tu, bali ifanyeni hukumu iliyo ya haki.*"

Wakati ambapo kuna muda lazima tuwe wazingatiaji wa kile wanachofikiria wengine, makadirio ya mwisho inahitajika kuangalia katika mahakama kuu. Wengine watasema "Acha dhamira yako iwe kiongozi wako." Lakini hebu tuchunguze…

Mahakama ya dhamiri ya mtu inayotoa maamuzi binafsi.

Mtazamo wa Paulo kuhusu "mahakama hii"…

1 Kor. 4:3, "*…wala sijihukumu hata nafsi yangu.*"

Hakika Paulo ahesabu hitaji la mtu kujichunguza mwenyewe.

Tunapaswa kujichunguza wenyewe wakati wa meza ya Bwana.

1 Kor. 11: 28-31, "*Lakini mtu ajihoji mwenyewe na hivyo aule mkate na kukinywea kikombe. Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu na nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili. Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu, na watu kadhaa wakadhaa wamelala. Lakini kama tungejipambanua nafsi zetu, tusingehukumiwa.*"

Lazima kila mara tuchunguze wokovu wetu.

2 Kor. 13:5, "*Jijaribuni wenyewe ya kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe, kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu? Isipokuwa mmekataliwa.*"

Kimsingi anasisitiza umuhimu wa dhamiri "njema".

- 1 Tim. 1:5, "*Walakini mwisho wa agizo hilo ni upendo utokao katika moyo safi na dhamiri njema, na imani isiyo na unafiki.*"
- 1 Tim. 1:19, "*Uwe mwenye imani na dhamiri njema, ambayo wengine wameisukumia mbali, wakaangamia kwa habari ya Imani.*"
- 1 Tim. 3:9, "*Wakiishika siri ya imani katika dhamiri safi.*"
- 1 Tim. 4:2, "*Kwa unafiki wa watu wasemao uongo, wakichomwa moto dhamiri zao wenyewe;*"

Lakini, katika swala lililoko kononi, Paulo alikataa kuitegemea "mahakama" hii.

Kusudi la mtazamo wa Paulo…

Alifahamu jinsi dhamiri ya mtu inavyoshindwa au makadirio binafsi inavyokuwa.

Mara nyingi alimtumikia Mungu kwa dhamiri njema.

Mdo. 23:1, "*Paulo akawakazia macho watu wa baraza, akasema, ndugu zangu mimi kwa dhamiri safi kabisa nimeishi mbele za Mungu hata leo hii.*"

Hata alipokuwa akiwatesa Wakristo.

Mdo. 26:9-11, "*Kweli mimi mwenyewe naliona ndani ya nafsi yangu kwamba yanipasa kutenda mambo mengi yaliyopingamana na jina lake Yesu Mnazareti; nami nikayafanya hayo Yerusalemu; niliwafunga wengi miongoni mwa Watakatifu ndani ya magereza nikiisha kupewa amri na wakuu wa makuhani; na walipouawa nalitoa idhini yangu. Na mara nyingi katika masinagogi yote naliwaadhibu, nikawashurutisha kukufuru; nikawaonea hasira kama mwenye wazimu, nikawaudhi hata katika miji ya ugenini.*"

Asipopata taarifa mtu anaweza akawa na dhamiri njema nab ado akafa katika kosa.

Paulo aliunga mkono uwezekano huo.

1 Kor. 4:4, "*Maana sijui sababu ya kuishitaki nafsi yangu;…*"

Wakati ambapo dhamiri yake ilikuwa safi, alifahamu kwamba haikumfanya awe sahihi.

Paulo alifahamu kwamba imebaki hukumu ya mwisho na isiyoshindwa…

Mahakama ambayo Kristo ndiye hakimu

Mtazamo wa Paulo kuhusu "mahakama" hii.

1 Kor. 4:4-5, "*Maana sijui sababu ya kujishitaki nafsi yangu, lakini sihesabiwi haki kwa sababu ya hiyo; ila anihukumuye mimi ni Bwana. Basi ninyi msihukumu neno kabla ya wakati wake, hata ajapo Bwana; ambaye atayamulikisha yaliyositirika ya giza, na kuyadhihirisha mashauri ya mioyo; ndipo kila mtu atakapoipata sifa yake kwa Mungu.*"

Kristo atawahukumu wanadamu wakati wa kuja kwake.

2 Kor. 5:10, "*Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya.*"

Alitazama hukumu ya Bwana kama ni zaidi, kwa sababu atafanya:

"*…kuleta katika nuru vitu vilivyofichwa katika giza*" (vitu ambavyo dhamiri njema inaweza kuvikosa).

"*…fanya ijulikane mashauri ya moyo*" (inafunua mambo ambayo maranyingi zimefichwa kutoka katika mtazamo wa wengine).

Hivyo, Paulo aliitazama "mahakama" hii kama ya mwisho, pasipo mahakama ya kidunia!

Kusudi la mtazamo wa Paulo.

Alifahamu kwamba hukumu ya Kristo ni lazima.

Kwa maana Mungu alitoa uthibitisho kupitia ufufuo wa Yesu.

Mdo. 17:31, "*Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu.*"

Na hivyo Paulo mara nyingi aliandika kuhusu hukumu yake.

- Rum. 14:10, "*Lakini wewe je! Mbona wamhukumu ndugu yako? Au wewe je! Mbona wamdharau ndugu yako? Kwa maana sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu.*"
- 2 Kor. 5:10, "*Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo*

aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya."

- 2 Tim. 4:1, "*Nakuagiza mbele za Mungu na mbele za Kristo Yesu, atakaye wahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake;*"

Alifahamu kwamba hukumu ya Kristo ilikuwa ni zaidi.

Alifahamu kwamba Bwana anaweza kufahamu siri za wanadamu.

- Yoh. 2:24-25, "*Lakini Yesu hakujiaminisha kwao; kwa kuwa yeye aliwajua wote; na kwa sababu hakua na haja ya mtu kushuhudia habari za mwanadamu kwa maana yeye mwenyewe alijua yaliyomo ndani ya mwanadamu.*"
- Mat. 9:4, "*Naye Yesu ali akijua mawazo yao, akasema, mbona mnawaza maovu mioyoni mwenu?*"

Hitimisho

Na hivyo tuna "Mahakama Tatu"…

- Mahakama inayoshughulika na wanadamu.
- Mahakama inayohuku kwa nafsi ya mtu.
- Mahakama ya hukumu ya Kristo.

Ni katika "mahakama" ipi tunashitakiwa kwa ajili ya tumaini ya wokovu.?

Je tumaini letu linaegemea katika kile ambacho wanadamu walioshindwa wamesema?

Je tumaini letu linaegemea katika kile tunachojisikia katika moyo wetu, au kwa kile ambacho dhamiri yetu inatuambia?

Au, tunaweka tumaini letu na taraja katika meneno ya Bwana ambaye atatuhukumu?

- Yoh. 12:48, "*Yeye anikataeye mimi asiyeyakubali maneno yangu, anaye amuhukumuye, neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho.*"
- Marko 16:16, "*Aaminiye na kubatizwa ataokoka asiyeamini atahukumiwa.*"
- Ufu. 2:10, "*Usiogope mambo yatakayokupata; tazama huyo ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na*

dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu mpaka kufa nami nitakupa taji ya uzima."

Nategemea kwamba tumeona kwamba kuna "mahakama" moja tu ambayo tunapaswa kuangalia kwa ajili ya jibu letu la mwisho kwa swali kama hilo, nay a kwamba kweli inatupasa tuwe na nia kama ya Paulo…

2 Kor. 5:9, "*Kwa hiyo tena ikiwa tupo hapa, au ikiwa hatupo hapa, twajitahidi kumpendeza yeye.*"